**Name:** _____________________________________________ **Adm No.:** ________ **Class:** __________

**KIDATO CHA PILI**

**KISWAHILI**

**MUDA: SAA 1¼**

**MAAGIZO**

1. ***Jibu maswali yote katika karatasi hii***
2. ***Maswali yajibiwe kwenye nafasi zilizoachwa***

**UFAHAMU (ALAMA 10)**

*Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali*

Pale kijijini petu hakuna mtu asiyemkumbuka Bwana Lopuya. Mkewe bwana huyu aliaga dunia wakati wa kujifungua, akamwachia mzigo wa kukilea kitoto ambacho hakikuwa kimenyonya hata tone moja la maziwa ya mamake.

Bwana Opuya alijizatiti na kujitolea kukilea kitoto kile. Alihiari kutopata bibi mwingine kwani alielewa kuwa mke mwingine asingemlea mwanawe kama mama mzazi. Aliamini kuwa mama wa kambo si mama.

Wanakijiji nao walimwonea Lopuya huruma. Zaidi ya kumwonea huruma, hamna jingine ambalo wangemsaidia kutahamaki wakaona kitoto kimekua mtu. Baba mtu naye akajitolea kadiri ya uwezo wake kumpa mwanawe malezi bora. Mtoto alipofika umri wa kwenda shule, baba yake akampeleka. Akatafuta vibarua huku na kule ili aweze kupata pesa za kuwakimu yeye na mwanawe. Mvulana naye alijitolea masomoni. Kichwa chake nacho kikawa chepesi. Kikapokea yote yaliyofundishwa. Kila mtihani alioufanya, kijana alikuwa anaongoza.

Baada ya elimu ya shule ya msingi, kijana yule akafaulu vizuri sana. Baba yake akazidi kujitolea katafuta karo. Kijana naye akapata elimu ya sekondari na kuhitimu kuendelea na masomo. Akajiunga na chuo kikuu kusomea taaluma ya uhasibu. Baada ya masomo, akaajiriwa na kampuni moja ya kimataifa. Kijana alioa na akabarikiwa kupata watoto wawili.

Wakati huo, uzee ulikuwa umepalia babake. Mzee huyu alihamia kwa mwanawe baada ya maradhi ya kupooza kumpata. Alitunzwa vizuri na mwanawe pamoja na mkewe. Watoto nao wakaibukia kumpenda babu yao sana. Kila mara wajukuu walipenda kukaa karibu na babu yao aliyewatolea hadithi za kusisimua.

Baada ya kipindi fulani mama watoto alianza kulalamika na kumwona mkwe wake kama mzigo. Alilalamika kuwa mzee alikuwa na mazoea ya kumwagamwaga chakula wakati wa kula na kuwa alikuwa anamwaibisha mbele ya marafiki wanapowatembelea. Bibi alitisha kuondoka pale iwapo mumewe hangemwondoa babake.

Ili kuleta suluhu nyumbani, waliafikiana wamhamishe mzee toka katika jumba kuu na kumweka katika kibanda kilichokuwa nje. La kushangaza ni kuwa mkazamwana alikuwa anampakulia mkwe wake katika vigae vya shani. Alilalama kuwa mzee alijuwa amemaliza sahani na vikombe vyake kwa kuviangusha na kuvivunja.

Wajukuu walishuhudia yote haya na hawakufurahishwa nayo. Wakawa wanamuuliza mama yao kuhusu mambo haya, naye hakuwapa jibu. Aliwakemea akiwachukulia kuwa ni watoto wadogo, nao wakanywea.

Siku moja wazazi waliwaona watoto wao wakiunganisha vigae vya sahani. Walifikiri kuwa huu ni mchezo wa kawaida wa watoto. Lakini walishindwa kujua kwa nini watoto walicheza bila kuwa na uchangamfu. Baba watoto akawauliza walichokuwa wakifanya. Wakajibu kuwa walikuwa wanaunganisha vile vigae vya sahani

ili wazazi wao watakapokuwa wazee kama babu yao, watakuwa wakiwapakulia chakula humo. Wazazi hao wakashtuka sana.

Walimwendea mzee, wakamwomba msamaha na wakaanza kumhudumia vizuri. Wajukuu nao wakajawa na furaha tena.

**Maswali**

1. Onyesha uamuzi wa Lopuya kuhusu mwanawe na sababu ya uamuzi huo (Alama1)

2. Fafanua mchango wa Lopuya katika malezi ya mwanawe (Alama2)

3. Taaluma ya uhasibu inahusu nini? (Alama1)

4. Mkazamwana alikuwa na malalamiko yepi dhidi ya mkwe wake (Alama2)

5. Makala haya yanatupa funzo gani? (Alama2)

6. Elezea matumizi ya maneno yafuatayo kulingana na muktadha wa Makala haya (Alama2)

    i) Kujizatiti

    ii) Vigae

**<u>MATUMIZI YA LUGHA (Alama 20)</u>**

a) Toa mifano miwili ya vikwaruzo (Alama2)

b) Taja ala mbili tuli za matamshi (Alama2)

c) Andika maneno yenye miundo ifuatayo (Alama2)
    (i) K + KI

(ii) KI +KI+KI

d) Onyesha viambishi awali na tamati katika neno lifuatalo: (Alama3)
Nilichokuachia

e) Andika matumizi mawili ya kikwaju/kishazari (Alama3)

f) Eleza maana ya mofimu (Alama1)

g) Taja aina mbili za mofimu (Alama2)

h) Ni nini maana ya shadda? (Alama2)

i) Nomino hizi ziko katika ngeli gani? (Alama2)
(i) Mtungi

(ii) Kamba

j) Tambua na ueleze vivumishi katika sentensi ifuatayo: (Alama1)
Mtoto wangu aliingia katika darasa lile.

k) Tambua aina za maneno katika sentensi ifuatayo (Alama3)

Tunda kubwa sana huuzwa bei ghali.

l) Andika sentensi hii katika usemi wa taarifa: (Alama2)
“Nitalima shamba mvua ikinyesha,” mkulima alisema.

m) Andika sentensi hii katika ukubwa (Alama2)
Chura huyo aliruka mtoni akazama.

n) Ni nini maana ya msemo “Enda mrama.” (Alama1)

o) Andika methali inayoafiki maelezo haya: (Alama1)
Hali ya mtu kuwa na hasira mara nyingi husababisha madhara.

p) Tunga sentensi yenye muundo ufuatao (Alama1)
T + E

**<u>ISIMU JAMII (Alama5)</u>**

Eleza majukumu matano ya lugha

**<u>FASIHI SIMULIZI (Alama5)</u>**

Taja aina tano za wahusika katika hadithi za kiswahili